**ISSN 0856 – 034X**

***Supplement No. 8*** ***24th February, 2017***

## *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 8 Vol. 98 dated 24th February, 2017*

Printed by the Government Printer Dar es Salaam by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA 32 la Tarehe 24/02/2017

(SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa Chini ya kifungu cha 89*

SHERIA NDOGO ZA (UVUNAJI WA MAJI YA MVUA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA, 2017

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Uvunaji wa Maji ya Mvua) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga za mwaka, 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo;

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo Hizi.

"Vifaa"maana yake ni vikinga maji (gutters)/bomba kutoka Kwenye vikinga maji kwenda kwenye tanki la kuhifadhia maji ya Mvua.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Mafinga.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Miundombinu ya maji" maana yake ni mfumo wa ukusanyaji maji ya mvua na kuyatunza katika chombo maalumu au tank kwa Matumizi ya baadae.

"Nyumba" maana yake ni jengo lililopauliwa kwa bati lenye lililokusudiwa kutumiwa na mtu/kikundi cha watu kwa ajili ya makazi, maskani, mastakimu, hashuo ama baiti.

"Taasisi" maana yake ni sehemu au idara au jumuiya ya Chuo kikuu au Wizara inayoshughulika na uchunguzi wa fani mbalimbali, au sehemu ya Idara au jumuiya ambayo inatoa Mafunzo maalumu.

"Shule" maana yake ni mahali ambapo wanafunzi hufundishwa elimu kama vile kusoma, kuandika, hesabu na masomo mbalimbali, ama ni eneo linalotumika kwa kufundisha na kujifunzia masomo mbalimbali, ama ni eneo linalotumika kwa kufundisha na kujifunza Mfumo rasmi wa elimu mbalimbali.

"Uvunaji maji ya mvua" maana yake ni kukusanya na kutunza Maji ya mvua kutoka kwenye paa la nyumba kwa kutumia teknologia rahisi ya makinga maji.

"Kiwanda" maana yake ni, jengo, banda, mahali ambapo Bidhaa mbalimbali hutengenezwa hapo,/mahali ambapo mafundi wanafanyia kazi zao ama eneo ambalo hutoa mafunzo.

"kibali cha ujenzi" maana yake ni idhini itolewayo na Halmashauri Kwa ajili ya ujenzi wa nyumba baada ya kuridhika na mchoro uliokidhi kiwango.

"Hotel" maana yake ni jengo maalumu ambapo chakula na vinywaji huuzwa humo na huduma ya kulala pia.

"Chuo" maana yake ni eneo ambalo hutoa mafunzo maalumu ya kazi fulani baada ya elimu ya msingi ama sekondari, kama chuo Kikuu, chuo cha ufundi, chuo cha kilimo na chuo cha ualimu.

Uvunaji wa Maji ya Mvua

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, chuo, taasisi,hoteli, kiwanda, ofisi na jengo lolote linalojengwa katika Halmashauri kuhakikisha linakuwa na miundo mbinu ya kuvuna maji ya mvua na kuyahifadhi katika Vyombo maalumu au matanki.

Mamlaka ya Halmashauri

5. Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuhakikisha kuwa kila mmiliki wa nyumba/taasisi/ chuo/ kiwanda/shule/hotel, iliyo ndani ya Mamlaka ya Halmashauri inaweka vifaa maalumu kwa ajili ya

kuvuna maji ya mvua.

Wajibu wa Mmiliki

6. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba/ taasisi/chuo/kiwanda/ shule/ hotel iliyopo ndani ya Halmashauri kuhakikisha Kuwa eneo lake lina vifaa vitakavyoweza kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua, kulingana na idadi ya watu watakao tumia jengo hilo.

Mchoro wa ujenzi wa miundombinu.

7. Kila mkazi wa Halmashuri ya Mji wa Mafinga ambaye anataka kujenga hotel, nyumba/kiwanda/taasisi/shule/ ndani ya Halmashauri atawajibika kuonyesha mchoro ambao utaonyesha ni kwa jinsi gani ameandaa miundombinu ya kuweza kuvuna maji ya mvua.

Uidhinishaji wa michoro.

8. Halmashauri haitaidhinisha mchoro wowote wa ujenzi wa jengo lolote endapo mchoro huo hautakuwa umeunganisha miundombinu ya kuvuna maji (gata)

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa

9. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote kukagua ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua.

Makosa

10. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote:

(a) Kutoonyesha katika mchoro wa jengo lake miundombinu na uwekaji wa vifaa vya kuvunia na kuhifadhia maji ya mvua na
(b) Kutoweka vifaa vya kuvunia maji ya mvua kwenye nyumba yake.
(c) Kuwasilisha ramani ya nyumba /jengo lake ili ipitishwe ikiwa haina michoro ya miundombinu ya uvunaji maji ya mvua
(d) Kushindwa kuweka vifaa vya kuvuna maji ya mvua katika jengo lake licha ya kuwa ramani yake ya ujenzi ilipitishwa na ikionyesha uwepo wa vifaa hivyo
(e) Kujenga nyumba/taasisi/hotel/kiwanda/shule/chuo au taasisi bila kuweka vifaa vya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa

faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kufifilisha kosa ikiwa mkosaji atakiri kufanya kosa hilo na baada ya kukiri kosa kwa hiari yake atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=)

JEDWALI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 12)*

Mimi ……………………………….………………………………. wa S.L.P …………. nakiri kupatikana na kosa la……………………………………..………..kinyume na Sheria Ndogo za Uvunaji wa Maji ya Mvua) za Halmashauri ya Mji wa Mafinga,2017. Nimekubali kulipa Tshs……………....................................................................................................... kama adhabu ya kosa hilo na nimepewa stakabadhi Na……………… ya tarehe…………………………

Sahihi ya Mkosaji…………………………………
Jina la mkosaji…………………………………….
Sahihi ya Afisa wa Halmashauri ya Mji……………………………………
Jina la Afisa wa Halmashauri ya Mji……………………………………….
Tarehe …………………………………………………………

Muhuri wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 29 Aprili 2016 na ilibandikwa mbele ya:

SAADA S, MWARUKA,
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji wa Mafinga*

CHARLES JOHN MAKOGA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Mji wa Mafinga*

NAKUBALI,

Dodoma,
9 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB.)
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*